



## **Mfuko wa Ukwasi**

Ni mfuko unatoa fursa kwa wawekezaji ambao wanahitaji kuwekeza fedha zao kwa kipindi kifupi au kirefu. Mfuko unawekeza kwenye masoko ya fedha tu. Hivyo kuwa na uwezekano mdogo wa mwekezaji kupoteza mtaji wake.

## **Lini nianze kuwekeza fedha zangu?**

Anza kununua vipande vya Mfuko wa Ukwasi mapema uwezavyo, utakavyoanza kuwekeza mapema ndivyo unapopata muda zaidi wa kuwekeza na kupata faida zaidi. Kila mwaka kiasi kitakachoongezeka (faida) kitazalisha faida nyingine katika miaka itakayofuata. Uwekezaji huu ni mfumo wa Faida Jumuishi (Compounding Interest)

## **Nani anayefaa kuwekeza katika mfuko wa Ukwasi.**

- Mtanzania mkazi na asiye mkazi.
- Vikundi, Kampuni, Asasi, Taasisi na Mashirika mbalimbali.

## Kwa nini Mfuko wa Ukwasi?

- **Usalama:** Uwekezaji mseto katika masoko ya fedha na dhamana mbalimbali
- **Faida:** Kuweka akiba na kukuza thamani ya fedha zako
- **Ukwasi:** Urahisi wa kupata sehemu au fedha zako zote ndani ya siku tatu (3) za kazi.
- **Uwazi:** Thamani ya kipande inatolewa kila siku ya kazi.
- **Gharama:** Mfuko unaendeshwa kwa gharama nafuu.
- **Kuratibiwa:** Mfuko unaratibiwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana.

## Kiwango cha kuwekeza.

Kiwango cha chini cha kuwekeza ni Shilingi milioni moja (100,000/) na kiwango cha chini cha nyongeza cha uwekezaji ni Shilingi elfu kumi (10,000/=) huku kukiwa hakuna kikomo katika kiwango cha juu cha uwekezaji.

## Mfano.

Uwekezaji wa miaka 10 ukionyesha faida kati ya asilimia 8 na 15

Faida inayotarajiwa	8%	10%	12%	15%
<b>Kiwango cha Awali</b>	5,000,000	5,000,000	5,000,000	5,000,000
<b>Miaka</b>	10	10	10	10
<b>Kiwango cha awali+Faida ya kawaida</b>	9,000,000	10,000,000	11,000,000	12,500,000
<b>Kiwango cha awali + Faida Jumuishi (compound)</b>	10,794,624.99	12,968,712.30	15,529,241.04	20,227,788.68
<b>Tofauti ya faida</b>	1,794,624.99	2,968,712.30	4,529,241.04	7,727,788.68

*Mahesabu haya yametokana na makisio ya ukuaji wa uwekezaji. Mapato ya uwekezaji yanaweza kuongezeka zaidi ya asilimia 15% au kupungua chini ya asilimia 8%.*

Yekeza Kwa  
jia Ya Simu

150\*82#

KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA UTT AMIS, S.L.P 14825, GHOROFA YA PILI JENGO LA SUKARI,  
MTAA WA SOKOINE NA OHIO, DAR ES SALAAM

Simu: +255 22 2122501 | Nukushi: +255 22 2137593 | Wakala: UTT MICROFINANCE • MATAWI YOTE YA BENKI YA CRDB NCHINI • MADALALI WOTE

WA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM. | Barua Pepe: uwekezaji@uttamis.co.tz | Tovuti: www.uttamis.co.tz |

Namba Za Bure +255 754 800 544 na +255 754 800 455 (VODA) +255 715 800 544 na +255 715 800 455 (TIGO) +255 782 800 455 (AIRTEL)



Tabadhariti: Thamani ya kipande inaweza kuongezeka au kupungua